JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Simu/Fax : 023 2628603
Barua pepe : **dakawatc@gmail.com**
Tovuti: www.datco.ac.tz

Chuo Cha Ualimu Dakawa
S. L. P. 944
MOROGORO.

Kumb. Na. ***DKWTC/JSTR/VOL.1/***

Tarehe 20/08/2018

Ndugu……..…….
S.L.P. ……..……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA ELIMU YA SEKONDARI KWA MWAKA 2018/2019

1.0 UTANGULIZI

Napenda kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada kuanzia mwezi **Oktoba 4, 2018**. Mafunzo haya ni ya muda wa miaka miwili (2). Ukiwa Chuoni utapatiwa muda wa kufanya Mazoezi ya kufundisha kulingana na kalenda ya chuo na maelekezo ya Wizara.

1.1 MAHALI CHUO KILIPO

Chuo hiki kipo **Mkoa wa Morogoro,** Wilaya ya Kilosa, Umbali wa kilometa **60** kutoka Morogoro Mjini, Barabara Kuu iendayo **Dodoma.**

1.2 NAMNA YA KUFIKA CHUONI

Ukifika Morogoro Stendi ya basi **MSAMVU** nenda stendi ya mabasi ya **Dodoma** panda magari madogo (Daladala au Noah), yaendayo **DUMILA** Shuka njia panda ya **VETA** chukua usafiri wa pikipiki wakulete chuo cha Ualimu Dakawa, umbali wa kilometa nne (**4)** tu toka njia panda nauli si zaidi ya **Tshs. 2,000/=** AU

Ukitokea Dodoma; Shuka njia panda ya **VETA** – kisha chukua pikipiki ikulete chuo cha Ualimu Dakawa, umbali wa kilometa nne (**4)** tu toka njia panda. Nauli ya pikipiki si zaidi ya **Tshs. 2,000/=**

Unashauriwa kufika Chuoni mapema kabla ya saa 11:00 jioni kwa ajili ya usalama wako

2.0 MAFUNZO

Chuo kitafunguliwa tarehe **04/10/2018** Unatakiwa kufika Chuoni tarehe **04/10/2018** bila kukosa. Iwapo utafika Chuoni baada ya tarehe **02/11/2018** hautapokelewa.

Ukiwa hapa chuoni katika kila Muhula utatakiwa kufanya mazoezi, majaribio, na Mitihani ya ndani na kufaulu. Utakapofika chuoni nenda kwa **Msajili** wa Wanachuo ambaye atakuelekeza taratibu zote za Chuo na kusajiliwa.

3.0 MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

3.1 Vyeti na Vitambulisho

Unatakiwa kuja na nyaraka zifuatazo ili usajiliwe

a) Barua ya kuitwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu (Joining Instruction)

b) **Vyeti HALISI** (Academic na Leaving Certificates) vya Kidato cha **Nne** / Kidato cha **Sita)**

d) Walioajiriwa walete barua kutoka kwa Waajiri wao ya kuruhusiwa Kuhudhuria mafunzo.

e) Vivuli **(photocopies)** vya vyeti vyako vyote.

f) Hakikisha umepimwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali na kujaziwa fomu iliyoambatanishwa kwenye barua hii ya kuthibitisha hali ya Afya yako.

g) paspoti size mbili.

3.2 ADA

Ada kwa mwaka ni **TShs. 600,000/=** ambayo inaweza kulipwa kwa mkupuo au kwa muhula Tshs. **300,000/=** Fedha hiyo Ilipwe kupitia **Akaunti Na**. **22101100214 - DAKAWA TEACHING COLLEGE A/C – NMB WAMI MOROGORO (*Pia Unaweza kulipia katika Tawi lolote la NMB Tanzania*)**

3.3 MICHANGO

Hakikisha unalipa michango yote ifuatayo kwenye

Akaunti Namba 01J1048471300; DAKAWA T.C - SELF RELIANCE A/C - CRDB. Mandela Branch Morogoro (*Pia unaweza kulipia katika Tawi lolote la CRDB nchini*)

Aina ya Michango	**Kiasi kinachotakiwa kulipwa (Tshs.)**
Huduma ya Kwanza	**5,000/=** kwa mwaka
Bima ya Afya ya Taifa	**50,400/** kwa wasio na Bima ya Afya
Usajili	**5000/=** inalipwa mara moja mwaka wa kwanza tu
Serikali ya Wanachuo	**5,000/=** kwa mwaka
Kukodi godoro	**20,000/** kwa mwaka
Tahadhari	**20,000/=** kwa mwaka
Kitambulisho	**5,000/=** kwa mwaka wa kwanza tu
Elimu ya Michezo	**10,000/=** kwa mwaka
Ulinzi	**15,000/=** kwa mwaka
TEHAMA (ICT)	**20,000/=** kwa mwaka
T-shirt yenye Nembo ya Chuo	**15,000/=** Inapatikana chuoni
Taaluma	**50,000/=** kwa mwaka
Usafi na Miundo Mbinu	**20,000/=** kwa mwaka
Ada ya Mtihani wa Taifa (NECTA)	**50,000/=** Inalipwa mara moja tu.
Mahafali	**15,000/=** kwa mwaka wa masomo
JUMLA	**305,400**

NB:- (i) Katika jedwali hapo juu hakikisha umelipa Tsh: 180,400/= kwa ambao hawana Bima ya Afya au lipa 130,000/= kama una Bima ya Afya.

Kwa muhula wa pili utatakiwa kulipa Tshs. 125,000/=

(ii) Uje na Kitambulisho cha Bima ya Afya kwa mwenye nacho.

(iii) Uje na **Bank P*ay* – *in* – *Slip*** kwa malipo yote hayo. Kumbuka kuandika **jina** lako kwenye **bank pay in slip** unapolipa fedha benki na uje na nakala halisi.

(iv) Fedha Taslimu Haitapokelewa na fedha ikishalipwa HAIRUDISHWI.

(v) Fedha za michango na Ada zisichanganywe kwenye akaunti moja

3.4 SARE YA CHUO

WANAUME

a) Suruali mbili za rangi nyeusi zenye mashono ya heshima,mifuko mitatu na rinda mbili.

b) Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya blue bahari (**Light blue)** yanapatikana chuoni. Uje na fedha Tshs **40,000/=** kwa ajili ya shati mbili (2)

c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika, vitavaliwa na soksi nyeusi wakati wote.

d) Tai ndefu nyeusi na koti jeusi (suti)

WANAWAKE

a) Sketi mbili nyeusi- ndefu zenye mashono ya pande sita (kitambaa cha suti cheusi)

b) Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya bluu bahari (**Light blue)** yanapatikana chuoni. Uje na fedha Tshs **40,000**/= kwa ajili ya shati mbili (2)

c) Tai fupi nyeusi (sio butterfly tie) na koti jeusi (Suti).

d) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye visigino vifupi vitakavyovaliwa na soksi nyeupe.

e) Watakaopenda kuvaa Hijab watumie rangi ya Light Blue (*Ifanane na shati*).

4.0 MAVAZI MUHIMU KWA WOTE.

a) Tracksuit ya bluu na raba pamoja na nguo nyingine za michezo kama bukta, fulana, sketi n.k

b) Mavazi mengine yote utakayokuja nayo, nje ya sare yawe ya mashono ya ***Heshima** na **yanayoakisi Taaluma ya Ualimu.***

5.0 MAHITAJI MUHIMU

5.1 MALAZI.

a) Blanketi, shuka mbili za light blue na foronya za light blue, mto pamoja na chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu.

b) Vyombo vya chakula –sahani, bakuli, kikombe **(visiwe vya plastic),** kijiko, galoni ya plastiki ya lita 5 ya kuhifadhia maji yako ya kunywa.

c) Ndoo ya kuogea. (*Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo)*

d) Shoka lenye mpini kwa **Wanaume** na Jembe lenye mpini kwa **Wanawake** kwa ajili ya usafi wa mazingira. Zingatia: Njoo na vifaa kwa jinsi yako kama ilivyoainishwa.

e) Tochi yenye betri kwa ajili ya tahadhari ya kukosekana kwa umeme.

f) Pazia light blue urefu wa ft. 9 kwa ft. 3.5 kwa ajili ya chumba chako.

g) Fedha kwa ajili ya matumizi yako binafsi

5.2 TAALUMA

a) Daftari kubwa zisizopungua 10 kwa muhula (Counter book Quire 2) *(hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo)*

b) Mihtasari na Vitabu vya kitaaluma vya kidato cha nne vya mchepuo uliochaguliwa.

c) Rimu **mbili** za karatasi. Moja nyeupe aina ya NO 1/mondi nyeupe (A4 photocopy paper) kwa ajili ya shughuli za Kiofisi na rimu ya pili yenye karatasi za mistari (Ruled rim paper) Hii ni kwa ajili ya karatasi za wanachuo za kufanyia mitihani. Rimu hizi mbili hutolewa kila mwaka *(Hupatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na chuo)*

d) Kwa Mwanachuo unechukua Somo la Hisabati uje na Scientific Calculator na Four Figure Table.

NB: Kumbuka kufika na sanduku imara lenye kufuli kwa utunzaji salama wa vifaa vyako vyote, pia kumbuka kuja na rimu moja kwa ajili ya matumizi yako binafsi

6. MWISHO:

Baada ya kusoma maagizo haya, iliyoambatanishwa na kukamilisha, ufikapo chuoni utakabidhiwa nakala ya Sheria, kanuni na taratibu za Chuo pia utatakiwa kukiri kukubali nafasi hiyo ya mafunzo kwa kujaza fomu

"***Ualimu bora huanzia chuoni; Tunakutegemea kuwa Mwalimu bora tangu mwanzo wa mafunzo yako"***.

KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU DAKAWA

DONALD M. GWILAJE
K/MKUU WA CHUO